Kuwa Kama Kristo

(Becoming Like Christ)

Na

Ellis P. Forsman

Kuwa Kama Kristo

(Becoming Like Christ)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 10, 2011

Kuwa Kama Kristo

Gal. 4:19

Gal. 4:19, "*Vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu;*"

Rum. 8:29, "*Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*"

2 Kor. 3:18, "*Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukirudisha utukufu kwa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*"

Agano jipya kwa wazi inatufundisha kuwa zaidi kama Yesu. Somo hili litazingatia vifungu vitatu vya maandiko ambazo zinatuimiza kuwa kama Kristo.

Kristo aumbike ndani yetu

Gal. 4:19, "*Vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.*"

Neno kuumbika "*morphoo*" inatumiwa katika Gal. 4:19 katika kumaanisha "kuhamishwa kwa Kristo." Maelezo: Paulo alitaka Wagalatia waruhusu Kristo aumbike ndani yao. Tunamitindo ambayo tunataka kujifanyia. Kama maumbo ya kimichezo, madaktari, wakulima, wachoraji, wajenzi, n.k. Zaidi ya yote nilazima tuwe kama Kristo.

Baadhi ya vitu ambavyo viliwazuia Wagalatia ili wasiwe kama Kristo:

- Gal. 5:4, "*Mmetengwa na Kristo ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema.*" (Wakishikilia Sheria ya Musa).
- Gal. 5:19-21, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, huzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.*" (Kukaa katika matendo ya mwili).

Uasherati – kufanya tendo la ndoa na mke au mume wa mtu mwingine.

Uzinzi – kufanya tendo la ndoa na mwingine, iwe mwenza wa mwingine au mtu ambaye hajaoa au kuolewa (Kamusi ya Vine).

Uchafu - tabia chafu, kihisia, tamaa.

Kukithiri kwa tamaa – kujibeza, kutorudi nyuma, tabia ya kutokuwa na aibu.

Gal. 5:15, "*Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana.*" (kuumana na kulana).

Paulo alichunguza vitu ambazo zinge wasaidia kuwa kama Kristo.

- Gal. 1:6-8, "*Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewatia katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.*" (kupokea injili katika usafi wake).
- Gal. 5: 22-24, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wamesulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.*" (Kuonyesha matunda ya Roho).
- Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai wala si mimi tena bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*" (Kumfanya Kristo uhai wao).

Kwa njia hii Kristo anaumbwa ndani yetu.

Tunapaswa kuhamishwa katika sura ya Kristo

Rum. 8:29, "*Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*"

Kuchaguliwa inatoka katika "*summorphos*" na hutumika katika kuchaguliwa kwa wana wa Mungu katika mfano wa Mwana wake.

Mungu ametuteua kwanza ili tufananishwe na mfano wa Mwana wake. Wale walioteuliwa kwanza ndio wale walioitwa na injili, wameitii na hivyo uhesabiwa haki.

Wale wanaoitwa na injili:

- Husamehewa na kuwa safi kama Kristo alivyo.
- Huitwa katika ushirika pamoja na Kristo. 1 Kor. 1:9, "*Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa nay eye mwingie katika ushirika wa Mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu.*"
- Sasa hufanana naye, wakiwa na sura yake.

Lazima tuhamishwe au kubadilika katika sura ya Kristo

2 Kor. 3:18, "*Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukirudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*"

Kugeuzwa hutoka katika neon *"metamorphoo*", kubadilika katika sura nyingine.

- Mat. 17:2, "*Akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru.*"
- Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza na ukamilifu.*"

Kwa kumfuata Kristo kama ilivyofunuliwa katika Agano Jipya tunageuzwa katika sura yake.

Hitimisho

Kazi yetu binafsi katika maisha haya ni kubadilisha maisha haya na kuyaweka katika maisha ya Kristo. Tunafanya hivyo kwa kufananishwa na Kristo miongoni mwetu, kwa kuhamishwa kuwa katika sura yake na kwa kubadilishwa au kufanya mabadiliko yo yote tunayohitaji katika maisha yetu.

Mtu anawezaje kugeuzwa na kuwa kama Kristo? Lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika elimu ya juu (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na yangu, akaniambia kwamba haamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nilichukua nafasi ya

kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kuwa kuishi maisha ya Ukristo ni vizuri, lakini hakuwa na uhakika kama anaamini kwamba kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba anahudhuria kanisani na kuishi maisha mema Mungu atamruhusu kwenda mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "Haiendi hivyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akwaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina ya Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kuna mwizi ndani ya nyumba yangu! Hivyo unachukua simu ya mkononi na kuwaambia polisi kuwa kuna mwizi ndani ya nyumba yako, na unawapa anwani yako. Ghafla, unasikia polisi wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, Samahani; Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadili maisha yake. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko ya tendo. Hivi ndio tunatakiwa kufanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba andiko hilo hapo juu linasema kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; siyo kwamba tayari mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndio haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kutimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia. Kubali hivi sasa kwakua ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi*

akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye." (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, na sio kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? *"…kwa ajili la ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe aaminiye **na** kubatizwa ataokoka, asiye amini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16).

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale lazima utufie. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katikia upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neon hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena,*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katikia damu ya Kristo ndani ya maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kwa kuunyunyizia udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujahamishwa kuingia kwa Kristo – fanyika mkristo, kwa nini usizingatie leo?